# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**NAIROBI SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

## NAIROBI SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**
**Karatasi ya 3**
**Mwongozo wa kusahihisha**

1. HADITHI FUPI : Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine- Ken walibora
   Hadithi ya Kanda la usufi – Rhoda Nyaga
   a) Muktadha wa dondoo
      i) Ni maneno ya mamake Sela
      ii) Kwa mzee Butali
      iii) Wako nyumbani kwao
      iv) Ni baada ya Sela kufukuzwa shuleni kwa sababu ya uja uzito na babake sela anawafukuza kutoka hapo kwake nyumbani.
      b) Tamathali iliyotumika
         Methali- uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi
   c) Sifa za msemewa- mzee Butali babake Sela
   - Mwenye hamaki/ hasira ghamidha- anakasirika sana baada ya kugundua sela ni mjamzito….Leo ndio mtanitambua"
   - Ni msikivu- alisikiza ushauri wa wazee, na pia wa mwalimu akawakubalia sela na mamake kurudi pale nyumbani, kumrudisha sela shuleni shuleni baada ya kujifungua

   - Msamehevu- baadaye anawasamehe sela na mamake na kuwaruhusu kurudi nyumbani
   - Ana msimamo dhabiti- hata baada ya kushawishiwa na mkewe, aliwafukuza pale nyumbani iliwabidi waende kwa majirani walipohifadhiwa.
   - Mtamaduni- anaamina malezi ya msichana ni wajibu wa mama. "……mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti?" alimuuliza mama sela
   - Mwenye hekima/ busara- alitambua umuhimu wa elimu ya watoto- akampeleka mwanawe shuleni licha ya umaskini uliowakumba.
   - Amewajibika kama mzazi- anampeleka sela shuleni na hata baaada ya kutambua uja uzito alikubali kumrudisha shuleni, na pia kulea mtoto wa sela
         d) Madhara ya mapenzi miongoni mwa wanafunzi
   - Mimba za mapema- sela anapata mimba akiwa shuleni.
   - Kukatiza masomo- ilibidi sela akatize masomo ili ajifungue
   - Mgogoro baina ya wazazi- mzee Butali anamfukuza mkewe na bintiye nyumbani, kumlaumu mkewe.
   - Huleta fedheha na uchungu kwa wazazi- mzee Butali aliona aibu na akachanganyikiwa asijue la kufanya. Kwa hasira anauliza mwalimu je, ni kwa nini sisi huwaleta watoto shuleni…..?
   - Sela na wenzake waliaibishwa na kuchekwa na wanafunzi wengine kwenye gwaride
- Watoto wanaozaliwa hawapati malezi ya watoto wao, halisi- Kadogo analelewa na Rozina, na wazazi wa sela.
- Maisha duni ya baadaye/ mkondo wa maisha wa wahusika kuvurugika- sela na masazu kutomudu utaratibu
  uliofaa ili kuhukua motto wa kutoka kwa wazazi wa Sela.
- Majuto- sela na pia masazu walijutia kwa matendo yao            Alama zozote 5x 2 = 10

2. Riwaya: Kidagaa kimemwozea Ken Walibora
   a) Sadifa

- Maelezo ya sadifa- utukiaji wa matukio mawili au zaidi kwa wakati mmoja bila kupangwa na kuathiri matukio ya baadaaye
- Kukutana kwa Imani na Amani kando ya ziwa mawewa wote wakiwa wamekosa matumaini katika maisha.
- Amani na Imani kupata kazi kwa ndugu wawili (Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu)
- Amani anaporudi kutoka hospitalini alimkuta Gaddafi na wenzake wakitaka kumuua Nasaba Bora na akamwokoa
- Amani kupewa kitabu kilichotokana na mswada aliokuwa ameandika yeye pamoja na vutabu vingine.
- Madhubutu kumkuta kijana Amani kwao nyumbani aliye na mawazo kama yake ya kuikomboa jamii yao ya Sokomoko kutokana na minyororo ya ukoloni mambo leo
- Amani kutaka kazi kwa Nasaba Bora na alipofika tu mchungani na mkamaji wake alikuwa 'mgonjwa'
- Mwalimu Majisifu kukaa kwa muda wa miaka kumi bila kuhusiana na mkewe kimapenzi akiogopa kupata vilema lakini siku aliyozidiwa na baridi na kulala na mkewe ilisadifu kuwa alipata mimba na kupata mapacha waliolemaa.
- Mashaka anachumbiana na Ben Bella mwanawe Maozi huku Nasaba Bora akiwa na uhusiano na Lowela Bintiye Maozi
- Imani alipopata barua ya Amani iliyohusu mswada ulioibiwa anaitwa na Dora na kuacha barua mezani na majisifu anaisoma na kuelewa kuwa Amani ndiye mwandishi wa ule mswada alioiba.
- Kinaya
- Nasaba Bora kulalamika nduguye Majisifu kuwa anautukanisha ukoo wao mtukufu- nyani haoni kudule
- Nyumbani kwa Imani kunaitwa 'Baraka' lakini tunaona akiandamwa na mikasa kama vile kufiwa na mamake, nyumba yao kuchomwa na shamba lao kuchukuliwa.
- Imani anajawa na tabasamu usoni daima ilhali moyoni anafundo la uchungu
- Ni kinaya kwamba dini zinahubiri amani undugu na rehema lakini maovu mengi hutendwa na wao kama vile kupigana
- Dj alihurumia lile jibwa Jimmy kwa kufungwa minyororo lingali gonjwa, linaishia kumshambulia baadaye
- Majisifu Nasaba Bora wamelelewa katika maadili ya kidini lakini wanaishia kutosikilizana
- Mwalimu majisifu anajibu maswali kinyume nay ale yaliyoandikiwa katika kitabu alochodai kukiandika.
- Kinaya kwa mwalimu majisifu kuacha pombe halali katika jokofu na kwenda kunywa pombe haramu kwa mama N'tilie kibandani.
- Ni kinaya Mtemi Nasaba Bora kutuma askari wakachome nyumba ya akina Imani badala ya kuwahakikishiia usalama
- Dj kupita karibu na kibanda cha Amani ule wakati anapowaza juu ya lile atafanya kuhusu kitoto Uhuru- anamtuma akaite Imani ili amsaidie                    Alama zozote 5x 2 = 10

3. a) Muktadha wa dondoo
   i) Ni maneno ya mtemi Nasaba Bora
   ii) Kwa mwalimu Majisifu
   iii) Ni nyumbani Majisifu alikuwa amemtembelea Nasaba Bora washauriane juu ya mambo kadha wa kadha na Mtemi akachukua fursa hiyo kumshauri majisifu dhidi ya ulevi wa kupindukia

   b) Tamathali ya usemi

   Kinaya –Mtemi Nasaba Bora anajivunia utukufu wa ukoo wao ilhali anajulikana kwa maovu kama vile- kuhusika katika mauti ya Chirchir Hanadi, wizi wa mashamba ukware

   c) Migogoro baina ya ndugu hawa

   i) Majisifu alikosa kihudhuria mkutano wa Nasaba Bora sikukuu ya uhuru
   ii) Mtemi Nasaba Bora anachukia ulevi wa kupindukia wa Mwalimu Majisifu
   iii) Mtemi Nasaba Bora amezoea kumzoea na kumkosoa kila wakati mwalimu Majisifu
   iv) Majisifu hakufuhia unafiki wa nduguye wa kijifanya anamjali yeye ilhali hajali maslahi ya wanasokomoko
   v) Majisifu anataka aachiliwe kuandama sela yake ya maisha/ mitazamo yao kimaisha ni tofauti

   d) Umuhimu wa Majisifu

- Ametumiwa kuangizia maudhui ya ughushi/ wizi wa mawazo yaw engine- ameiba na kuchapisha miswada isiyo yake.
- Ni kielezo cha wsomi wanaoshindwa kuyamudu maisha yao- elimu yake haijamwezesha kuthibiti uraibu wa ppombe haramu
- Ametumiwa kubainisha taasubi ya kiume- anamwachia mkewe malezi ya watoto na shughuli zote za nyumbani
- Ni mfano wa wazazi wanaowadharirisha watoto wanyonge- anawatekeleza hata kutaka kuwaua watoto wake walemavu
- Ametumiwa kubainisha ubaguzi wa kinasaba/ kikabila- majisifu anapozembea kazi na kufutwa, bado anapewa ualimu kwa sababu anajulikana kwa viongozi- 'zimwi likujualo halikuli…'
- Mfano wa viongozi wa umma wasiowajibika kazini- muhula mzima hajaenda kazini kufunza
- Ametumiwa kubainisha unafiki- anahimiza mashoka kusoma kwa bidii ili ajiendeleze kimasomo ilhali haendi shuleni kuwafundisha
- Ametumiwa kuonyesha umuhimu wa kusameheana na kuwa na maridhiano anamsamehe ndugu yake na kufanya juhudi ili Yusuf aondolewe lawama za mauaji pawe na maridhiano

4. Tamthilia: Mstahiki Meya T. Arege
    a) Muktadha
        i) Ni maneno ya Gedi
        ii) Akimwambia mstahiki Meya
        iii) Ni ofisini mwa meya
        iv) Meya alikuwa akipokea maji aliyokuwa ameagiza ili anywe na akahisi harufu, aliyodharau ilitokana na maji hayo, na akitaka kujua iwapo Gedi alikuwa na hakika kuwa si hayo maji yaliyotoa harufu
    b) Mambo yaliyopelekea kuwepo kwa harufu hiyo
        i) Wafanyikazi wamegoma
        ii) Takataka imerudikana
        iii) Kuna uhaba wa maji mjini
    c) Umuhimu wa mzungumzaji- Gedi

- Ametumiwa kuangazia udikteta wa Meya- anatumwa kuwaelezea waandamanaji kuwa watafutwa kazi na wengine waajiriwe.
- Ametumiwa kama kielelezo cha ukoloni- mambo leo Meya anafurahi sana anapopigiwa saluti na kuita 'sir' kila anapomuita
- Ametumiwa kuangazia ubarakala- ni miongoni mwa vibaraka wa meya ambao wako tayari kufanya lolote ili wamfurahishe meya\
- Kupitia kwake tunafahamishwa kwa nini wageni wanaotarajiwa hawazi kufika- wafanyikazi wa uwanja wa ndege pia wamegoma kuwaunga wenzao mkono
- Kupitia kwa Gedi tunafahamishwa hatima ya wageni- wangetua mji wa shwauara.
- Anaangazia ufisadi wa meya- aliajiri mhazili ambaye hakustahili hiyo ajira- pia yeye hajafika kazini
- Kupitia kwake tunafahamishwa kwamba wafanyikazi wa bahari ya mafuta pia wamegoma kuwaunga mkono wafanyikazi wa baraza
- Hali ya maji kukosa maji na mahoteli kukosa maji imeangaziwa kupitia kwake

    d) Harufu ni ishara ya uozo:

- Ufisadi: mfano Meya na Mwanakadarsi kupanga kuibia baraza kupitia kesi mahakamani
- Uongo: meya kudanganya dawa zimeagaziwa
- Unafiki wa kidini: meya kujificha katika dini ili kuficha uovu wake, mhubiri kumuunga mkono badala ya kuukashifu uovu wake.
- Ubainifu wa mali ya umma: meya kujistarehesha na marafiki katika mahoteli, anapanga kutumia mabilioni kuwafurahisha wageni.
- Ubinafsi- meya kuwapeleka watoto wake kusomea ng'ambo badala ya kuboresha sekta ya elimu na ya afya

- Utabaka- meya na madiwani kuishi maisha ya kifahari huku wafanyikazi wakitopea katika lindi la umaskini uliokithiri
- Matumizi mabaya ya Askari- wanatumwa kuwakomesha na kuwatawanya wanapoandamana na kulalamika
- Wizi wa mali ya umma- meya ananyakua viwanja vya umma
- Kutowajibikia kwa viongozi kutunza mazingira hadi cheneo na njaa na ukame.

5. UKOLONI- MAMBO LEO
    - Maelezo ya ukoloni mambo leo, ukoloni unajitokeza baada ya nchi kujinyakulia uhuru na wenyeji wenyewe
    - Utegemezi- bado mji wa cheneo unategemea mataifa ya nje kufadhili mipango ya maendeleo katika nchi yao- mameya wanaotarajiwa kuzuru cheneo
    - Utawala wa meya unatumia mamilioni ya pesa kuwaandalia mameya kutoka ng’ambo katika mahoteli ya kifahari ingawa wana nakisi katika bajeti.
    - Utawala wa meya unaagiza vinywaji na vyakula kutoka nje na dawa pia zimeagizwa kutoka nje.
    - Utawala wa meya unapuuza mipango ya maendeleo ya miaka kumi ya mji wao huku ukujidai kufuata na kudhamini malengo ya maendeleo ya milema.
    - Meya kuppeleka bibi kujifungulia ng’ambo na watoto wake kusomea huko ili wapate uraia wa huko kwa imani kuwa huko ni kuzuri zaidi ya kwao.
    - Ubinafsi wa meya wa kunywa maji ya chupa peke yake si uafrika una asili katika uzungu
    - Viongozi kuendeleza utabaka/ kujitenga na raia wa kawaida
    - Nyumbani kwa mmeya kumepambwa na samani makochi na zulia la kupendeza
    - Meya kupenda kutumia lugha ya kizungu mfano ‘bllody hen, nonsense”

   b) Unafiki katika tamthilia ya mstahiki Meya

- Maelezo ya unafiki- kujifanya au kujisingizia uadilifu/ wema/ uongofu ilhali uhalisi wako kinyume kabisa kwa mawazo na vitendo.
- Viongozi kuwahadaa wananchi kuwa baraza la cheneo ndilo lenye uthabiti mkubwa likilinganishwa nay ale mengine yaliyolinzuka ilhali limekumbwa na mizozo ya wafanyikazi
- Mhubiri kujifanya mcha Mungu na kudai kuwa ana wito wa kuhubiri
- Bili kumshawishi meya kukubali kukutana na viongozi wa wafanyikazi lakini awafanye waonekane kama ndio hawataki suluhisho
- Meya kujifanya kujali maslahi ya walinda usalama, madiwani na kuwaongezea mishahara, kuwaondolea kodi ilhali nia yake ni kuahonga ili wamuunge mkono.
- Meya anawakanya askari dhidi ya kuwaua na kuwaumiza waandamanaji kwani huu ni mwaka wa uchaguzi
- Meya kudai kuwa cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano- ilhali watu wanakufa njaa, hawawezi kuyamudu mahitaji ya kimsingi
- Meya kuwaandalia madiwani kifahari ilhali wana nakisi katika bajeti na wanatarajiiaili kuendeleza mipango yao

6. Fasihi simulizi
   a) Kuigiza ni hali ya kuiga matendo, tabiia za watu/ viumbe
      Sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na matendo.
   b) Vipera vya maigizo
      -Michezo ya jukwaani
      -Michezo ya watoto
      -Vichekesho
      -Miviga
      -Majigambo
      -Ngonjera
      -Matambiko
      -Ngoma

-Ngomezi

c) Sifa za muigizaji bora

-Jasiri/ mkakamavu
-Mbunifu- anatumia mbinu mbalimbali ili kuvutia
-Mwenye ujuzi wa kutumia ishara za uso, miondoko inayoana na hali anazoiga
-Mwenye uwezo wa kubadili toni na kiimbo kubainisha hali tofauti za matukio
-Mwenye ukwasi na ufasaha wa lugha
-Aweze kuwashirikisha hadhira yake vyema mwenye ufahamu na utamaduni wa hadhira yake ili asije kuiudhi kwa maneno au ishara
-Mfaraguzi- aweze kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake.
-Anayeilemea hadhira yake vyema mwenye ufahamu na utamaduni wa hadhira yake ili asije kuiudhi kwa maneno au ishara

d) Vikwazo vya maigizo

-Kukosa mahali pa kuigizia
-Kukosa wakati wa kuigiza
-Uhaba wa maleba yanayofaa
-Kukosa uewzo wa waledi wa lugha

-Kukosa kuelewa ujumbe unaowakilishwa

7. Ushairi

a) Shabaha ya mtunzi wa shairi hili kuwatetea wanyonge wanaoghulumiwa na wenye nguvu japokuwa ndio wazalishaji/ kupinga vita unyanyasaji wanaofanyiwa wanyonge

b) Aina za bahari katika shairi hili

i) Msuko- mshororo wa mwisho ni mfupi/ mizani chache
ii) Tarbia/ unne- kila ubeti una mishorooro mine
iii) Ukara- vina vya ukwapi vinabadilikabadilika lakini vya mwisho ni sawa 'yo'
iv) Sakarani- shairi limechanganya bahari kadha pamoja
v) Ukawafi- mishororo ya kwanza mitatu imegawa vipande viatu/ ina vina vitatu

c) Mbinu zilizotumiwa kutimiza mahitaji ya kiarudhi katika shairi

i) Inkisari/ ufupishaji wa maneno
Tavumiliaje badala ya nitavumiliaje
Kwacho badala ya kwa hicho
Vumiliyo badala ya kuvumiliana
Kwayo badala ya kwa hayo
Wanotulimiya badala ya wanaotulimia
Ndo badala ya ndio
Wanaumiya badala ya waoumia

ii) Mazida/ kurefusha maneno
Wawapo badala ya wapo
Nalije badala ya lije

iii) Tabdila/ kubadili sauti za maneno- wanotulimiya badala ya wanaotulimia
Mamiya badala ya mamia
Angamiyo badala ya angamio
Tuling'owe badala ya tuling'oe

iv) Kuboronga/ kufinyanga sarufi
'wanyonge yawakutayo badala ya yanayowakuta wanyonge

v) Kwayo sina zuiliko badala ya sina la kinizuia
Hawa sioni wengine badala ya sioni wengine ila hawa

d) Ujumbe katika ubeti wa kwanza

i) Hatavumilia kuendelea kuona wanyonge wakidhulumiwa

ii) Ameamua kutangaza katika maandishi kwa vyovyote vile

e) Sura ya shairi

i) Lina beti tano

ii) Lina mishororo mine kila ubeti

iii) Mshororo wa mwisho umefupishwa

iv) Mishororo ya kwanz mitatu ina migao mitatu/ vina vitatu

v) Mizani za mishororo ya kwanza mitatu ni 2, 6, 8= 8

f) Mambo yanayomkera mshairi

**i)** Wanyonge waghulumiwa

**ii)** Wazalishaji ndio hunyanyaswa

**iii)** Wanyonge ndio hukumbwa na maafa

**iv)** Wanyonge ndio huwapa mamlaka/ nguvu viongozi

**v)** Wenye nguvu wametawaliwa na tama/ ubinafsi/ uchoyo

g) Maana ya

i) Zuiliko- kizuizi/ pingamizi/ kikwazo/ kisiki

ii) Mauko- madhila/ maangamizi/ shida/ madharau